

CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA



S.L.P 1125, DODOMA Simu: 026 – 2961101, Nukushi: 026 – 2961100, Barua pepe:
info@lgti.ac.tz& Tovuti: www.lgti.ac.tz

Kumb. Na: LA.32/201/01/142

08 Desemba 2020

ZABUNI NA PA/080/2020/2021/NCS/04 YA UPANGISHAJI WA VYUMBA VYA BIASHARA

1. Chuo cha Serikali za Mitaa kinawatangazia na kuwakaribisha kuleta maombi wafanya biashara/kampuni/Taasisi/Watu binafsi wenye uwezo wa kupanga vyumba vya maduka ya biashara vilivyopo Chuo cha Serikali za mitaa Hombolo na Dodoma mjini area C

NA	AINA YA BIASHARA	IDADI YA VYUMBA VILIVYOPO	ENEO KILIPO CHUMBA CHA BIASHARA	KAMPASI
1.	Biashara ya kuuza shajala(stationery)	2	Jengo la mgahawa wa zamani	Hombolo
2.	Biashara ya kuuza shajala(stationery)	3	Karibu na ukumbi wa mhadhara I&II	Hombolo
3.	Biashara ya saluni(saloon)	1	Jengo la Mnong'ono	Hombolo
4.	Duka la rejareja(Retail shop)	1	Jengo la Mnong'ono	Hombolo
5.	Biashara ya kuuza shajala(stationery)	1	Ndani ya jengo la kituo	Dodoma mjini area C
6.	Mgahawa wa chakula	1	Eneo la wazi ndani ya kituo	Dodoma mjini area C

2. MASHARTI YA ZABUNI

- Mwombaji anapaswa kulipa ada ya Zabuni ambayo ni Tsh 30,000/= kupitia **CONTROL NUMBER** atakayoipata ofisi ya Uhasibu Chumba Namba,jingo la utawala,Ada hiyo haitarudishwa.
- Mwombaji anapaswa kutaja kiasi atakacholipa Chuo cha Serikali za Mitaa kama kodi ya pango kwa mwezi.

- iii. Mwombaji awe na leseni hai ya biashara anayoomba kufanya,Cheti cha utambulisho wa mlipa kodi (TIN) au nakala ya kodi ya ongezeko la thamani(VAT).
- iv. Mwombaji anaweza kuomba kama mtu binafsi/kikundi/Taasisi au kampuni.Kama muombaji ni kampuni,kikundi au taasisi anapaswa kuambatanisha nakala ya hati ya usajili.
- v. Mwombaji anapaswa kuambatanisha nguvu ya sheria (power of Attorney)
- vi. Mwombaji asiwe na mashauri katika chombo chochote cha sharia kuhusiana na mkataba wa aina yoyote na Taasisi yoyote ya Serikali.
- vii. Mwombaji atakayeshinda atapaswa kukilipa chuo cha Serikali za Mitaa kodi ya miezi minne ndani ya siku saba tangu apewe barua ya tuzo.
- viii. Mwombaji haruhusiwi kuomba chumba cha Biashara Zaidi ya kimoja kwenye aina ya Biashara husika.
- ix. Mwombaji asiwe anadaiwa kodi na Chuo cha Serikali za Mitaa.

3. Kwa maelezo na ufafanuzi Zaidi wasiliana na Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni S.L.P 1125 Dodoma kuanzia saa 2:30 asubuhi mpaka saa 9:30 Alasiri(jumatatu-ijumaa) isipokuwa siku za mapumziko.

Barua za maombi zitumwe kwa anuani ifuatayo:

KATIBU,

BODI YA ZABUNI CHUO CHA SERIKALI ZA MITAA,

S.L.P 1125,DODOMA.

4. Nyaraka za maombi ziwe na nakala halisi moja iliyofungwa kwa LAKIRI,landikwe juu ya bahasha" NAMBA NA JINA ZABUNI INAYOOMBWA" NA ZIKABIDHIWE KWENYE OFISI YA Katibu wa Bodi ya Zabuni.
5. Mzabuni anashauriwa kutembelea eneo analoomba kupanga kabla ya kujaza maombi ya zabuni,kutokufanya hivyo itakuwa ni hasara yake mwenyewe.
6. Siku ya mwisho ya kuwasilisha maombi ya zabuni ni siku ya Juma tano,Tarehe 16/12/2020 kabla ya saa Nane na nusu mchana(8:30).Zabuni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Zabuni,waombaji wote au wawakilishi wao wanaalikwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni hizo utakaofanyika siku hiyo katika ukumbi wa Maktaba ya Chuo cha Serikali za Mitaa.

7. Chuo cha Serikali za Mitaa hakitalazimika kukubali/kutokukubali kutoa zabuni kwa mwombaji yeyote kutokana na kigezo cha malipo makubwa/malipo kidogo ya zabuni.
8. Zabuni zitakazochelewa kuwasilishwa, zabuni za kielektroniki na zabuni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji zabuni, kwa hali yoyte ile hazitakubaliwa kwa tathmini.



Magdalena Z. Katunzi

K.N.Y. MKUU WA CHUO

08/12/2020

Kny: Mkuu wa Chuo
Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo
S. L. P. 1125,
DODOMA